Mtandao Wa Sala Wa
Baba Mtakatifu Ulimwenguni
TANZANIA

eym EUCHARISTIC YOUTH MOVEMENT VIJANA WANA EKARISTIA

Waraka wa Sala wa Mwezi Oktoba 2026

NIA ZA SALA ZA BABA MTAKATIFU

Kila mwezi, Baba Mtakatifu huukabidhi Mtandao wake wa Sala Ulimwenguni nia za sala. Nia hizi hutuelekeza kujiunga naye katika kujali utu na utume wa kanisa. Nia hizi ni wito kwa ulimwengu wote kuziweka sala zetu katika matendo mahsusi; ni dira ya utume wa huruma kwa ulimwengu.

Nia ya Sala ya Papa, Oktoba 2026:

Kwa ajili ya utume wa afya ya akili.:

Tusali ili kwamba huduma ya kichungaji ya afya ya akili ianzishwe katika Kanisa lote, na kusaidia kuondokana na unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wenye magonjwa ya kiakili.

SALA YA MWEZI OKTOBA 2026

Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

Mungu wa uzima,
Unajua mioyo yetu kwa ndani kabisa,
unajua nuru na giza vilivyomo ndani yetu,
na majeraha ya siri ambayo wakati mwingine hakuna anayeyaona.

Leo tunawaleta mbele yako ndugu zetu
wanaopambana na changamoto za afya ya akili,
wanaoteseka peke yao kwa wasiwasi, sonona, au aina nyingine ya ugonjwa wa akili.
Kwa upole, unawaita kwa majina,
na ndani yako wanarudishiwa tena utu na tumaini.


Ee Bwana, tusamehe kwa nyakati tulipowageuzia kisogo wenzetu hawa,
tukichochea unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya wenye matatizo ya afya ya akili.
Lifanye Kanisa lako liwe nyumba iliyo wazi,
mahali salama ambapo kila mtu anapata nafasi—
jumuiya inayoandamana na kila mtu na isiyomtenga yeyote,
inayosikiliza bila kuhukumu na inayokwenda karibu na wote bila hofu.

Tunakusihi, Bwana, kwa wale wanaowatunza wenye changamoto hii:
wataalamu, wanafamilia, na wanaojitolea—
wanaume kwa wanawake, ambao, kwa saburi na upendo,
wanajenga madaraja ya uelewa na faraja.
Wakirimie nguvu na huruma waendelee kuhudumia wengine.

Tushushie Roho wako Mtakatifu,
ili tujifunze kupokea na kujumuisha huduma ya afya ya akili
katika maisha na utume wa jumuiya zetu na Kanisa lote,
na hivyo kuwa ishara hai ya huruma yako,
huruma isiyokoma kamwe, bali daima inaendelea kurejesha hali njema. **Amina**

popesprayer@aorjesuits.org
WhatsApp +255 766333833 | Phone +255 754865401
www.salinapapa.org | www.popesprayer.va | www.clicktopray.org | www.thepopevideo.org

MTAZAMO WA MWEZI OKTOBA, 2026



Mwezi huu Baba Mtakatifu anatusihi tusali ili huduma ya afya ya akili ianzishwe katika Kanisa lote. Tunapaswa kutambua kwamba bado kuna maeneo mengi ambapo hata Kanisa halijafahamu kikamilifu changamoto zinazokabili katika eneo la afya ya akili. Papa ametuhimiza tukabiliane na hali hii moja kwa moja, uso kwa uso.

Idadi ya watu wanaojiua duniani inafikia 700,000 kila mwaka, kwa mujibu wa Shirika ya Afya Duniani, WHO. Kwa kila tukio moja la kujiua lililokamilika, inakadiriwa kuwa kuna kati ya majaribio 20 hadi 30 ya kujiua. Mengi ya haya yanahusiana na matatizo ya afya ya akili, na unyanyapaa unaoendana nayo.

Unyanyapaa unaozunguka masuala ya afya ya akili bado ni kikwazo kwa utambuzi wa mapema na matibabu. Zaidi ya kupokea matibabu haya, jumuiya zetu zinapaswa kusaidia kukuza mazungumzo na kupokea ukweli huu, hivyo kushinda unyanyapaa na ubaguzi wa aina yoyote. Sala kwa wale wanatenga muda na upendo wao katika juhudi hii ni msaada usio na mbadala.

SALA YA MAJITOLEO YA KILA SIKU

Ee Baba mwema,
natambua uko hapa pamoja nami.
Nakuja mbele yako katika siku hii mpya.
Weka moyo wangu kwa mara nyingine tena karibu na Moyo wa Mwanao Yesu,
anayejitoa kwa ajili yangu na anayekuja kwangu katika Ekaristi.
Roho wako Mtakatifu anifanye kuwa rafiki na mtume wake,
aliye tayari kwa utume wake wa huruma ulimwenguni.

Ninaweka mikononi mwako furaha na matumaini yangu,
kazi zangu na maumivu yangu, mimi mzima na kila kitu nilichonacho,
kwa kushirikiana na kaka na dada zangu wa Mtandao huu wa Sala Ulimwenguni.

Pamoja na Mama Maria, ninakutolea siku yangu kwa ajili ya utume wa Kanisa
na kwa nia ya Sala ya Baba Mtakatifu [na Askofu wangu] kwa mwezi huu. **Amina**.

MTANDAO WA SALA WA BABA MTAKATIFU ULIMWENGUNI

Mtandao wa Sala wa Papa Ulimwenguni ni Kazi ya Kipapa iliyokabidhiwa kwa Shirika la Yesu (Wajezuiti). Tupo katika zaidi ya nchi 90, tukijenga jumuiya ya kiroho yenye zaidi ya watu milioni 22 wanaotafuta kuishi kila siku wakiwa tayari kwa utume wa Mungu.

Sehemu muhimu ya maisha yetu ni **nia za sala Baba Mtakatifu za kila mwezi za Papa**, ambazo zinatazama, kusali na kutenda tukizikabili changamoto kubwa ubinadamu na Kanisa. Nia hizi zinatusaidia kuona, kuhisi, na kutumikia kwa moyo kama wa Yesu. **WEWE** pia unakaribishwa katika familia hii.

popesprayer@aorjesuits.org
WhatsApp +255 766333833 | Phone +255 754865401
www.salinapapa.org | www.popesprayer.va | www.clicktopray.org | www.thepopevideo.org